REDD+ SES℠
Social & Environmental Standards

Viwango vya Kijamii na Kimazingira vya MKUHUMI+

Toleo la Juni 2010

Vigezo vya kusaidia uundaji na utekelezaji wa programu za MKUHUMI+ zinazoongozwa na serikali ambazo zinaheshimu haki za Jamii yawatu asilia na jamii nyingine iliyoko hapo kisheria na kuongeza manufaa muhimu zaidi yakijamii na kimazingira.

www.redd-standards.org

Toleo hili la viwango vya mazingira na kijamii vya MKUHUMI+ vimetokana na warsha ya wadau mbalimbali iliyofanyika Copenhagen kuanzia tarehe 5-7 Mei 2009, majadiliano na wawakilishi wa serikali na asasi zisizo za kiserikali yaliyofanyika Nepali tarehe 29 Juni mpaka tarehe 3 Julai na majadiliano yaliyofanyika Tanzania kuanzia tarehe 9-11 Septemba, maoni ya umma yaliyopokelewa katika kipindi cha maoni ya kwanza ya jamii kuanzia tarehe 2 Oktoba hadi 30 Novemba 2009 (pamoja na michango kutoka kwenye majadiliano yaliyofanyika Ecuado tarehe 22-26 Oktoba), maoni yaliyopatikana kwenye mkutano wa Kamati ya Viwango uliyofanyika Copenhagen tarehe 4-5 Disemba 2009 pamoja na maoni ya umma yaliyopokelewa kipindi cha pili kuanzia tarehe 15 Januari hadi 16 Aprili 2010 (ikijumuisha michango kutoka mikutano ya wadau katika ngazi ya kitaifa na ya kijamii nchini Liberia 8-12 kwanzia tarehe Machi, na katika ngazi ya kijamii nchini Nepali tarehe 10 Machi na Tanzania tarehe 13 Machi)

Viwango hivi vimeandaliwa kwa njia inayohusisha serikali, asasi zisizo za kiserikali na asasi zingine za kiraia, asasi za jamii, taasisi za kisera za kimataifa na taasisi za utafiti na sekta binafsi. Kamati ya Viwango inayowakilisha kwa usawa wajumbe ndiyo inayosimamia uandaaji wa viwango hivi. Wengi wa wajumbe wa kamati hii wanatoka katika nchi ambazo MKUHUMI utatekelezwa kwa kutambua kwamba serikali na asasi za kiraia kutoka katika nchi hizi, ndio watakaongoza utekelezaji wa viwango hivi. Mchakato wa kuandaa hivi viwango unawezeshwana Climate, Community & Biodiversity Alliance (CCBA) na CARE International.

Toleo hili la viwango linatekelezwa kwa majaribio katiya mwaka 2010 na 2011. Maoni yoyote na mapendekezo ya maboresho au nyongeza kwenye toleo hili la viwango yanakaribishwa. Tafadhali weka jina lako, jina la taasisi, kumbukumbu namba ya kanuni-vigezo-kiashiria husika, maoni yako na mapendekezo ya mabadiliko katika rasimu hii. Maoni yapelekwe kwa jdurbin@climatestandardsorg na yatapewa kipaumbele kwenye awamu ya mapitio ya viwango inayofuata mwaka 2011. Fomu ya kupeleka maoni, nakala za viwango kwa Kiingereza, Kifaransa, Kispanishi na Kipotugizi na taarifa kuhusu historia na mchakato wa uandaajii wa hivi viwango vinapatikana katika tovuti ya http://www.climate-standardsorg/REDD+/

Umuhimu wa viwango

Wakati shughuli zinazopunguza utoaji wa gesi zinazotokana na ukataji wa misitu na uharibifu wa misitu (MKUHUMI) na zinazochangia katika uhifadhi, usimamizi endelevu wa misitu na kuongeza akiba ya kaboni katika msitu (MKUHUMI+) vinauwezo wa kuleta manufaa/faida kubwa za kijamii na kimazingira, shughuli nyingi pia zimeonyesha hatari kubwa, hususan kwa jamii ya watu asilia na jamii iliyopo kisheria na hasa walioko pembezoni[1]na/au waishio hatarini[2] na makundi ya jamii yanayotegemea misitu hii. Kwa kutambua kuongezeka kwa uelewa katika ngazi za kimataifa na kitaifa kuhusu mahitaji ya hifadhi madhubuti za kijamii na kimazingira, juhudi hii ina lenga kuelezea na kujenga mhimili kwa ajili ya ngazi ya juu ya utendaji wa kijamii na kimazingira kutoka kwenye programu za MKUHUMI+.

Majukumu ya viwango

Jitihada hii inatengeneza viwango ambavyo vinaweza kutumika na serikali, asasi zisizo za kiseriakli, wakala wa fedha na wadau wengine kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza programu za MKUHUMI+ ambazo zitaheshimu haki za watu wa asili ya eneo husika na wanajamii na kuleta faida kubwa za kijamii na kibaioanuai. Viwango hivi vimetengenezwa ili vifanye kazi kwa ajili ya mfumo mpya wa kiulimwengu wa MKUHUMI+ unaotegemewa kuibuka kutokana na mazungumzo ya UNFCCC (Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kudhibiti Mabadiliko ya Tabia Nchi) na mchakato wa majadiliano unaohusiana na yanayoendelea, yaani kwa ajili ya programu za serikali zinazotekelezwa katika ngazi ya kitaifa au nchi/baadhi ya nchi kwa pamoja na kwa ajili ya aina zote za malipo yanayotegemea masoko na yale yanayotegemea mfuko maalumu uliotengwa. Kwa kutoa mwongozo uliokamilika kwa ajili ya kushughulikia masuala nyeti yanayohusiana na matokeo ya kijamii na kimazingira ya program za MKUHUMI+, Viwango hivi vinatoa maelekezo ya kusaidia kuunda MKUHUMI+ na pia kusaidia mfumo wa kutoa taarifa za matokeo ya kijamii na kimazingira ya program za MKUHUMI..

Vipengele vya viwango

Viwango vina kanuni, vigezo na viashiria ambavyo vitaainisha mambo yenye mashaka na ngazi ya utendaji wa kijamii na kimazingira vinavyohitajika.

- **Kanuni** ni viwango vya ‘madhumumi’ ambavyo vinafafanua malengo ya viwango na kuainisha kwa upana. Hizi kanuni ni matamko muhimu kuhusu matokeo yanayotarajiwa na hazijatengenezwa ili zihakikiwe.
- **Vigezo** vinatoa masharti ambayo yanapaswa kutimizwa ili kufanikisha kanuni. Inaweza kuhakikiwa moja kwa moja lakini vinaelezewa kwa undani zaidi na viashiria.**Viashiria** ni maeneo yenye ukomo wa yanayoelezeka kwa maneno na kwa takwikimu ambazo

[1] ‘Watu au makundi ‘waliopembezoni’ ni wale ambao wanaushawishi mdogo san juu ya ufanyji wa maamuzi. Upembezoni unaweza kuhusishwa na sababu kama jinsis, ukabila, hali ya kiuchumi na dini. Viwango vya kijamii na kimazingira vya MKUHUMI+ kwa uwazi kabisa unachukua njia tofauti ambayo inalenga kua ainisha na kushughulikia hali ya upembezoni kwa kila namna.

[2] ‘Makundi ya watu walioko hatarini’ ni wale ambao hawana rasilimali za uhakika kwa ajili ya maisha endelevu (za kijamii, kiutamaduni, watu, kifedha,maliasili, miundombinu na kisiasa) na/au wameandamwa sana na matatizo na mishtukoya nje ikiwemo mabadilio ya tabia nchi, ambayo yanaathiri rasilimali hizi na/au uwezo wa watu kuzitumia rasilimali hizi. Utegemezi wa misitu ni moja ya sababu zinazoathiri hali hii ya uhatari hususan pale ambapo programu ya MKUHUMI+ yenyewe itakavyobadili upatikanaji wa rasilimali za misitu. Mara nyingi hali ya upembezoni inazidisha na hali ya uhatari mfaano kuwapemebzoni kwa sababu ya jinsia.

zinaweza kupatikana na kuhakikiwa kwa kufuata kigezo ili kuonyesha kwa vi**tendo kama** vigezo vimeweza kufuatwa:-

Katika ngazi ya kanuni na vigezo viwango ni sawa katika nchi zote. Katika ngazi ya viashiria, kuna mchakato wa ki inchi wa kutafsiri[3]ili kutengeneza viashiria ambavyo vimetengenezwa kulingana na mazingira ya nchi husika. Ili kuongoza huu mchakato katika nchi husika wa kutengeneza viashiria, “muongozo wa viashiria” ulio sawa kwa nchi zote umetengenezwa. Mchako wa kimataifa wa ukaguzi utahakikisha usawa kwenye tafsiri katika nchi.

Ufuatiliaji, kutoa taarifa na kuhakiki

Kuna chaguo mbalimbali zinazofikiriwa kwa ajili ya ufuatiliaji, utoaji taarifa na uhakiki (MRV) ambazo zitaleta usawa katika ushiriki na umiliki wa wadau na kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji wakati huohuo kutoa moyo wa kuboresha utendaji. Kwa vishiria, mchakato wa MRV utahusisha nchi husika.

Maelezo juu ya Programu ya MKUHUMI+

i. Tamko la malengo
ii. Utambuzi wa visababishi vya ukataji wa miti hovyo na uharibifu wa misitu
iii. Unaelezea sera, hatua, shughuli na mipango ya uundaji na utekelezaji.
iv. Kuainisha maeneo ya kijiografia ambapo shughuli zitakuwa zinafanyika na patakapo faa
v. Kuainisha mpangilio wa kitaasisi kwa ajili ya kupanga program, utekelezaji na tathmini.

[3] Tafsiri kwa nchi maalum ina maanisha tafsiri katika ngazi ya utawala unaoongoza programu ya MKUHUMI+

Kanuni 1: Haki ya kumiliki ardhi, maeneo na rasilimali[4]zinatambulika na kuheshimiwa[5] na programu ya MKUHUMI+	
Kigezo	**Muongozo wa Viashiria[6]**
1.1 Programu ya MKUHUMI+[7] inawatambua kwa ufasaha wenye haki[8]mbalimbali (kisheria na kimila[9]) na haki zao kumiliki ardhi, maeneo na rasilimali muhimu kwa ajili ya programu	1.1.1 Mchakato shirikishi unaanzishwa wa kumbukumbu na kutambua ardhi za kisheria na kimila zilizopo, maeneo na haki za kumiliki/kutumia/kupata/kusimamia rasilimali muhimu kwenye programu ikiwemo haki ya wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu ikiwemo haki zingine zozote zinazoweza kuleta mgongano 1.1.2 Mipango ya matumizi ya ardhi ikiwemo mipango[10] ya usimamizi wa misitu kwenye maeneo yaliyomo kwenye program ya MKUHUMI+ inatambua haki za watu wote muhimu[11]na mipaka yao pamoja na haki zingine zinazoweza leta mgongano
1.2 Programu ya MKUHUMI+ inatambua na kuheshimu haki zote za kisheria na kimila[12]za ardhi, maeneo na rasilimali ambazo jamii ya watu asilia ya eneo husika au wanajamii[13] wamekuwa wakimiliki, wameshikilia au kutumia au kujipatia[14]	1.2.1 Sera za program ya taifa ya MKUHUMI+ inahusisha kutambua na kuheshimu haki za kimila za watu wenye wa asili ya eneo husika au wanajamii 1.2.2 Mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na mipango ya usimamizi wa misitu kwenye maeneo yaliyomo kwenye programu ya MKUHUMI+ inatambua na kuheshimu haki za kimila na kisheria za watu wenye asili ya eneo husika na wanajamii

[4] 'Rasilimali'inaelewekakujumuisha huduma za mfumo ekologia zinazotolewa na rasilimali hizi
[5] 'Heshima' inachukuliwa kujumuisha na sio kudharau au kunyima haki.
[6] Muongozo huu wa viashiria unaainisha vipengele muhimu kwa kila kigezo. Kutakuwa na mchakato wa tafsiri kwa nchi maalum kuandaa viashiria vinavyoendana na nchi husika.
[7] Programu ya MKUHUMI+ inajumuisha malengo, sera na hatua zilizokwisha tayarishwa kwa ajili ya programu na sera nyingine zinazosaidiana nazo
[8]Inajumuisha wenye haki binafsi na jamii ya watu asilia na wengine wenye haki za ujumla
[9]Haki za kimila za kumiliki ardhi na rasilimali itamaanisha ardhi ya jamii iliyokuwa ya muda nrefu na matumizi ya rasilimali kulingana na sheria za kimila, maadili, tamaduni za watu asilia na jamii wengine pamoja na matumizi ya mzunguko kuliko hati rasmi ya kisheria ya kumiliki ardhi na rasilimali inayotolewa na serikali
[10] Kutambua kwamba mipango ya matumizi ya ardhi na usimamizi wa misitu ilioandaliwa chini ya programu ya MKUHUMI+ inapaswa kuandaliwa kwa ushirikishwaji uliokamilika wa wadau na wenye haki wote kwa kulingana na kigezo 6.2
[11] Wenye haki muhimu wameainishwa na programu ya MKUHUMI+ kwa kulingana na kigezo 6.1
[12] Ikijumuisha haki binafsi na za jumla
[13]Popote maneno Jamii ya watu asilia na jamii iliopo kisheria yatakapotumika katika viwango hivi, ni muhimu kwamba msisitizo utakuwa unaelekezwa kwa watu walioko pembezoni na/au makundi yalioko hatarini katika jamii hizi.
[14]Kutambua kwamba watu asilia wana haki ya kumiliki, kutumia, kuendeleza na kushikilia ardhi, maeneo na rasilimai ambazo wamepata kwa sababu ya umiliki wa kimila au matumizi mengine ya kimila, pamoja na yale ambayo wamepata kwa njia nyingine

	1.2.3 Programu ya MKUHUMI+ inaendeleza kulinda haki za kisheria15 za ardhi, maeneo na rasilimali ambazo watu wenye asili ya eneo husika au wanajamii wamekuwa wakimiliki, kushikilia au kutumia au kujipatia kimila.
1.3 Programu ya MKUHUMI+ inahitaji hali ya uhuru katika uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia kwa Jamii asilia na jamii nyingine kwa ajili ya shughuli yoyote itakayo athiri haki zao za kumiliki ardhi, maeneo na rasilimali	1.3.1 Sera za programu ya MKUHUMI+ unasimamia kanuni ya hali ya uhuru katika uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia kwa Jamii asilia na jamii nyingine kwa ajili ya shughuli yoyote itakayo athiri haki zao za kumiliki ardhi, maeneo na rasilimali 1.3.2 Programu ya MKUHUMI+ kwa uthabiti inasambaza taarifa juu ya hitaji la kuwa na hali ya uhuru katika uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia kwa Jamii asilia na jamii nyingine kwa ajili ya shughuli yoyote itakayo athiri haki zao za kumiliki ardhi, maeneo na rasilimali 1.3.3 Wenye haki kwa ujumla wanaainisha mchakato utakaohakikiwa katika hatua za wao kupata hali ya uhuru katika uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia pamoja na kuainisha wawakilishi wa taasisi zao za asili ambazo zina mamlaka ya kutoa ridhaa kwa niaba yao. 1.3.4 Hali ya uhuru katika uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia inapatikana kutoka kwa Jamii asilia kwa kufuata mila na desturi, kanuni za jamii hiyo kwa shughuli yoyote itakayo athiri haki zao, hususan haki zao za kumiliki na kusimamia ardhi inayomilikiwa kiasili, mipaka na rasilimali. 1.3.5 Hali ya uhuru katika uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia inapatikana kutoka kwa wanajamii kwa ajili ya shughuli yoyote itakayo athiri haki zao za kimila za umiliki wa ardhi, mipaka na rasilimali kufuatana na taratibu zinazokubalika 1.3.6 Pale ambapo kuhamishwa au kuhama ama kwa makazi au kiuchumi inapotokea kwa kutokana na hali ya uhuru katika

[15] Inajumuisha kupata haki za kisheria zilizopo na kubadilisha haki za kimila kuwa haki za kisheria

	uelewa na kuwa na taarifa kabla ya kuridhia kunakuwa na makubalino ya awali juu ya upatikanaji wa ardhi mbadala na/au fidia iliyo ya haki, na haki ya kurudi pale ambapo sababu za kuhamishwa zimekoma.
1.4 Programu ya MKUHUMI+ inatambua na kutumia mchakato kwa ajili ya utatuzi madhubuti wa migogoro juu ya haki ya ardhi, maneneo na rasilimali zinazohusiana na program hii na program haiendelei na shughuli yoyote ambayo itaharibu matokeo ya mchakato wa utatuzi wa mgogoro huo	1.4.1 Mbinu madhubuti na yenye uwazi inapatikana kwa ajili ya kusuluhisha migogoro juu ya haki za ardhi, mipaka na rasilimali zinazohusiana na program za MKUHUMI+ zinaainishwa na kutengenezwa. 1.4.2 Migogoro juu ya haki ya ardhi, maeneo na rasilimali iliyoletwa na program ya MKUHUMI+ inatatuliwa kwa uwazi ndani ya muda uliokubalika. 1.4.3 Hakuna shughuli yoyote itafanyika na programu ya MKUHUMI + ambayo itaathiri matokeo ya mgogoro ambao haujatatuliwa juu ya haki ya ardhi, mipaka na rasilimali inayohusiana na programu
1.5 Pale ambapo programu ya MKUHUMI+ inawezesha umiliki binafsi[16] wa haki ya hewa ukaa[17], haki hizi zinatokana na haki ya kisheria na kimila za ardhi, maeneo na rasilimali[18] ambazo zimezalisha upungazaji wa uzalishaji wa gesijoto	1.5.1 Pale ambapo programu ya MKUHUMI+ inawezesha umiliki binafsi wa haki ya hewa ukaa, haki hizi zinatokana na miliki ya kisheria na kimila ya ardhi, mipaka na rasilimali zilichangia upunguzaji wa kuzalisha kwa gesi joto

Kanuni 2: Manufaa ya programu ya MKUHUMI+ yanagawanywa kwa usawa[19] miongoni mwa wahusika wote[20] wenye haki na wadau[21]	
Vigezo	Muongozo wa viashiria
2.1 Gharama zinazotarajiwa,	2.1.1 Gharama na mapato na manufaa mengineyo

[16] Umiliki wa haki zinazotokana na hewa ukaa zinaweza kuwa kwa mtu binafsi au kwa ujumla

[17] Haki ya hewa ukaa' zitainishwa kama haki za kuweza kuingia mikataba na vipengele vya manunuzi/malipo kwa ajili ya kuhamisha umiliki wa upunguzaji wa uzalishaji wa gesi joto au kuondoa na uendelezaji wa viwango vya hewa ukaa vilivyopo

[18] Haki za kisheria na za kimila za umiliki wa ardhi, maeneo na rasilimali kwa wanaohusika na wenye haki katika programu ya MKUHUMI+' wameainishwa kulingana na kipengele cha 1.1

[19] Uswawa' na 'usawa katika mgawanyo' vinamaanisha kuwa na mlingano na haki kw wahusika wote

[20] 'wenye haki na makundi ya wadau husika' wameanishwa na programu ya MKUHUMI+ kulingana na kigezo 6.1

[21] Wenye haki husika' ni wale ambao haki zao zinatarajiwa kuathiriwa na programu ya MKUHUMI+ na 'wadau' ni wale ambao maslahi yao yataathiriwa kwa njia moja au nyingine na program.

manufaa yanayotegemewa na hatari zinazoambatana[22] na programu za MKUHUMI+ zimeainishwa kwa ajili ya wenye haki husika na makundi ya wadau[23] katika ngazi[24] zotekwa kutumia mchakato shirikishi.	yanayotarajiwa, pamoja na hatari zinazoambatana na programu za MKUHUMI+ zimechambuliwa kwa kila mwenye haki husika na vikundi vya wadau katika kila ngazi kwa kutumia mchakato shirikishi.
2.2 Mifumo iliyo wazi, shirikishi, thabiti na yenye ufanisi[25] imeanzishwa kwa ajili ya usawa katika mgawanyo wa manufaa yatokanayo na programu ya MKUHUMI+ miongoni na baina ya wenye haki na vikundi vya wadau husika kwa kuzingatia gharama, manufaa na hatari zinazoambatana nazo.	2.2.1 Kuna ushiriki thabiti na uliokamilika[26] wa wenye haki na wadau husika ambao wanataka kuhusishwa ikiwemo watu wasio kuwa na fursa na/au makundi ya watu waishio hatarini miongoni mwao katika kuainisha mchakato wa kufanya maamuzi na mfumo wa kugawana manufaa kwa usawa miongoni na baina ya wenye haki na vikundi vya wadau husika. 2.2.2 Programu ya MKUHUMI+ inatumia njia inayoshirikisha na mchakato uliyowazi unaohitaji watu wa jamii asilia na jamii nyingine wakiwemo wasiopata fursa na/au watu waliohatarini kati yao, kuamua namna mapato yatakavyo fanywa, jinsi yatakavyo tolewa na jinsi gani yataweza kuboresha uhakika wa maisha yao kwa muda mrefu. 2.2.3 Sera zilizowazi na miongozo ya mgawanyo wa manufaa imetayarishwa, imekubalika, imesambazwa kwa walengwa na imetekelezwa. 2.2.4Taratibu za utawala na usiamamizi wa fedha na mgawanyo wa manufaa zinafanyika kwa wakati na kwa gharama nafuu. 2.2.5 Muundo wa mfumo wa mgawanyo wa manufaa umetokana na kupitiwa kwa fursa mbalimbali kwa kuzingatia usawa, uthabiti[27] na ufanisi wa programu ya MKUHUMI+ 2.2.6 Mchakato wa mgawanyo wa manufaa unajumuisha taratibu

[22] Uchambuzi wote wa gharama, manufaa na hatari vijumuishe zile ambazo ni za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja na zijumuishe masuala ya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi. Gharama zijumuishe za zile za ukosaji. Gharama zote za manufaa, na hatari ziringanishwe kutokana na hali halisi ambayo inaonekana katika matumizi ya ardhi kama programu ya MKUHUMI+ isingekuwepo.

[23] 'Wenye haki husika' na vikundi vya wadau' vimeainishwa kwa kulingana na kigezo 6.1.

[24] Katika ngazi ya chini, kitaifa na ngazi nyingine zinazohusika

[25] Ufanisi' unamaanisha kuwa kufikia shabaha kwa gharama, juhudi na muda kidogo

[26] Ushirikishwaji ulio thabiti na uliokamilika' unamaanisha ushawishi wa maana kwa wenye haki na wadau husika wanaotaka kuhusisha katika hatua zote na kuhakikisha wanapata taarifa kwa wakati.

[27] Uthabiti' wa programu ya MKUHUMI+ unamaanisha kiwango ambacho upunguzaji wa hewa ukaa na malengo mengine yamefikiwa.

	zilizo wazi na zinazopatikana za kuwasilisha na kutatua malalamiko
2.3 Kuna ufuatiliaji wa gharama na manufaa ya programu ya MKUHUMI+ ulioshirikishi na wa wazi ikiwemo mapato yoyote na mgawanyo wake baina ya wenye haki na wadau husika.	2.3.1 Wenye haki na wadau husika wakiwemo wawakilishi wa wasio na fursa na/au makundi ya watu waishio katika hatari wanashiriki kikamilifu katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mchakato wa mgawanyo wa manufaa uliokubalika katika ngazi za kitaifa na za chini. 2.3.2 Wenye haki na wadau husika wakiwemo wawakilishi wa wasio na fursa na/au makundi ya watu waishio katika hatari wanashiriki kikamilifu katika utoaji wa taarifa na kuzipitia gharama, mapato na manufaa mengine na jinsi jamii ilivyogawanywa kwa kuzingatia uchambuzi wa awali wa gharama zinazotarajiwa, manufaa yanayotegemewa na hatari[28] zinazoambatana nazo.

Kanuni 3: Programu ya MKUHUMI+ inaboresha usalama wa maisha[29] kwa kipindi kirefu na maisha bora kwa jamii asilia na jamii nyingine kwa kuangalia zaidi jamii walio na mahitaji zaidi	
Vigezo	**Muongozo wa viashiria**
3.1 Programu ya MKUHUMI+ inazalisha zaidi athari chanya na za muda mrefu za u uhakika wa maisha na maisha bora kwa jamii ya watu asilia na jamii nyingine kwa kuzingatia watu wenye mahitaji na hatarini zaidi.	3.1.1 Malengo ya programu ya MKUHUMI+ yanajumuisha kubooresha uhakika na usalama wa maisha ya jamii asilia na jamii nyingine kwa muda mrefu kwa kuzingatia watu wenye mahitaji na hatarini zaidi.3.1.2 Watu ambao wako hatarini zaidi wameainishwa miongoni mwa jamii asilia na jamii nyingine zinazoshiriki katika program ya MKUHUMI+ 3.1.3 Jamii asilia na jamii nyingine ikiwemo watu ambao wako hatarini zaidi miongoni mwao, wanakili kuwa wamepata manufaa kutokana na kushiriki kwenye programu ya MKUHUMI+ 3.1.4 Programu ya MKUHUMI+ inazalisha rasilimali zaidi[30] ili kubooresha uhakika wa maisha ya jamii asilia na jamii nyingine kwa muda mrefu.

[28] Mchakato wa awali wa gharama za zilizotarajiwa, manufaa yanayotegemewa n aharai zinazoambatana nazo kwa kila mwenye haki na makundi ya wadau yanazingatiwa kulingana na kigezo 2.1.

[29] Uhakika wa maisha' yanategemea dhamana za kijamii, kiutamaduni, kibinaadamu, maliasili, na uwezo wa kifisikia na kisiasa.

[30] Rasilimali zinatakiwa kuongezeka ukilinganisha na hali halisi ambayo ni matumizi halisi ya ardhi kwa wakai huo kama programu ya MKUHUMI+ isingekuwepo.

	3.1.5 Hatua zinachukuliwa ili kuhakikisha kuwa uhakika wa maisha na ubooreshaji wa maisha unaleta manufaa kwa jamii ya watu asilia na jamii nyingine na ni endelevu
3.2 Kuna tathmini shirikishi ya athari chanya na hasi za kijamii, kiutamaduni, haki za kibinadamu, kimazingirana kiuchumi za programu ya MKUHUMI+ kwa ajili ya jamii ya watu asilia na jamii nyingine pamoja na athari zinazotabiriwa na zilizotokea.	3.2.1 Mchakato shirikishi umeundwa na kutekelezwa ili kutathmini athari chanya na hasi zilizotabiriwa na zilizohalisi za kijamii, kiutamaduni, haki za binadamu, kimazingira na kiuchumi za programu ya MKUHUMI+ kwa ajili ya jamii ya watu asilia na jamii nyingine hasa watu walio katika hatari zaidi miongoni mwao ikijumuishwa athari zinazotofautishwa kwa jinsia. 3.2.2 Ufuatiliaji wa athari za kijamii, kiutamaduni, haki za binadamu, kimazingira na kiuchumi unachukua hatua ya kutofautisha na ambayo inaweza kuainisha athari chanya na hasi kwa watu walio hatarini zaidi zikiwemo athari zinazotofautishwa kwa jinsia.
3.3 Programu ya MKUHUMI+ inatumika kwa kufuata tabiri na tathmini za athari zinazoendelea ili kupunguza athari hasi na kuendeleza athari chanya na za muda mrefu , na atahari za kuboresha maisha na maisha bora kwa jamii ya asilia na jamii nyingine	3.3.1 Hatua za kuanzisha na na kupunguza kwa uthabiti zaidi athari hasi kwa jamii ya watu asilia na jamii nyingine kwa ujumla na hasa kwa watu walioko hatarini zaidi wanajumuishwa katika uandaaji wa programu ya MKUHUMI+[31] 3.3.2 Mrejesho kutokana na ufuatiliaji unatumika kuandaa na kutekeleza hatua za mbele za kupunguza athari hasi zinazoweza kujitokeza hasa kwa watu walioko katika hatari zaidi wakati wa hatua za utekelezaji wa programu ya MKUHUMI+.

Kanuni 4: Programu ya MKUHUMI+ inachangia katika malengo mapana ya maendeleo endelevu na utawala bora[32]	
Vigezo	**Muongozo wa viashiria**
4.1 Programu ya MKUHUMI+ inachangia kufikia malengo ya sera za maendeleo endelevu,	4.1.1 Programu ya MKUHUMI+ inafafanua namna sera na hatua zake zitakavyochangia kwenye utekelezaji wa sera zilizopo za kupunguza umaskini, mikakati na mipango

[31] Kwa kutambua kuwa hatua zozote za kukabili katika programu ya MKUHUMI+ zinapaswa kuandaliwa na kutekelezwa kwa ushirikishwaji uliokamilifu kwa wenye haki na wadau husika kwa kuangalia kigezo 6.2

[32] Vipengele vya utawala bora vinajumuisha upatikanaji, ushirikishwaji wa watu, uwazi, uwajibikaji, utawala wa sheria, utabirikaji, upatikanaji wa haki na uendelevu.

mikakati na mipango[33]ilioanzishwa katika ngazi za kitaifa na ngazi nyingine husika.	iliyoanzishwa katika ngazi ya taifa na ngazi nyingine husika za serikali. 4.1.2 Programu ya MKUHUMI+ inafafanua namna sera na hatua zake zitakavyochangia kwenye utekelezaji wa sera za bioanuwai zilizopo, mikakati na mipango[34] iliyoanzishwa katika ngazi ya taifa na ngazi nyingine husika za serilaki 4.1.3 Ustawi wa jamii kitaifa, umaskini na ufuatiliaji wa malengo mengine ya maendeleo ya milenia yanaonyesha kubooreshwa katika maeneo ambapo programu ya MKUHUMI+ inatekelezwa.
4.2 Programu ya MKUHUMI+ inapelekea maboresho katika utawala wa sekta ya misitu na sekta nyingine zinazohusika	4.2.1 Programu ya MKUHUMI+ inaainisha masuala ya utawala wa misitu kwa upana ambayo yanaweza kushughulikiwa hususan yale yanayohusiana na usawa[35], uthabiti na ufanisi wa programu ya MKUHUMI+ na kuanzisha shabaha maalumu za utekelezaji kitaifa. 4.2.2 Programu ya MKUHUMI+ inajumuisha kujengea uwezo taasisi na hatua nyingine zinazolenga kubooresha masuala ya kiutawala. 4.2.3 Mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa programu ya MKUHUMI+ ina viashiria muhimu vya utawala wa misitu.
4.3 Programu ya MKUHUMI+ inachangia katika kuheshimu na kulinda haki za binadamu.	4.3.1 Programu ya MKUHUMI+ inafafanua namna sera zake na hatua zitakavyochangia kuboreshaheshima na ulinzi wa haki za binadamu. 4.3.2 Mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa Programu ya MKUHUMI+ una viashiria muhimu vya haki za binadamu
4.4 Kuna utayari mkubwa wa serikali juu ya programu ya MKUHUMI+ katika nchi zao.	4.4.1 Muundo wa kitaasisi ya programu ya MKUHUMI+ unaendana na uongozi wa serikali 4.4.2 Taasisi za serikali/mashirika yanaongoza katika uandaaji, utekelezaji na tathmini ya programu ya MKUHUMI+
4.5 Programu ya MKUHUMI+ inaendana na sera ,mikakati na mipango katika ngazi zote husika na kuna utaratibu thabiti	4.5.1 Vipengele vya mipango ya matumizi ya ardhi katika programu ya MKUHUMI+ pamoja na utambuzi wa haki za kimila kwenye mipaka ya ardhi na rasilimali zinaenda sambamba na michakato mingine ya mipango ya matumizi

[33]mfaano; mikakati/shabaha upunguzaji wa umaskini, bajeti za kitaifa, mikakati ya bioanuwai ya kitaifa, mikakati ya taifa ya mabadiliko ya tabia nchi, mipango ya mabadiliko n.k.

[34] Ikijumuisha maeneo ya umma, binafsi na yanayolindwa kijamii

[35] Usawa na usawa usio na upendeleo vinamaanisha ile tu kutopendelea upande wowote pamoja na watu walio pembezoni na makundi yalioko hatarini.

baina ya serikali na taasisi nyingie zinazohusika na uundaji, utekelezaji na tathmini ya program ya MKUHUMI+ na mashirika na taasisi nyingine za serikali husika	ya ardhi. 4.5.2 Programu ya MKUHUMI+ inaendana na sera za kitaifa na mikakati ya kulinda haki za binadamu na kupigana na ubaguzi dhidi ya makundi yaliyopembezoni. 4.5.3 Programu ya MKUHUMI+ inaingizwa katika mwongozo wa sera ya sekta ya misitu na sekta nyingine husika. 4.5.4 Tofauti zilizopo kati ya programu ya MKUHUMI+ na sera husika za maendeleo endelevu, utawala, na haki za binadamu mikakati na mipango zinaainishwa na kushughulikiwa. 4.5.5 Mchakato wa kupitia na muda maalum wa kushughulikia tofauti zilizopo baina ya programu ya MKUHUMI+ na sera zingine za maendeleo endelevu, mikakati, na mipango umeanzishwa na kutekelezwa. 4.5.6 Mchakato uliothabiti na wenye ufanisi umeanzishwa kuunganisha programu ya MKUHUMI+ na wizara zote husika na taasisi/mashirika ya kiserikali yanayohusika katika ngazi zote.

Kanuni 5: Programu ya MKUHUMI+ inaendeleza na kubooresha[36] bioanuwai na huduma za mifumo huduma za ikolojia[37]	
Vigezo	**Muongozo wa viashiria**
5.1 Bioanuwai na huduma za mfumo ekolojia zinazoweza kuathiriwa na programu ya	5.1.1 Bioanuwai na huduma za mfumo ekologia[38] ambazo zitaathiriwa na programu ya MKUHUMI+ zimeanishwa, kupewa kipaumbele na kuwekwa katika ramani[39] katika

[36] Athari kwenye bioanuwai na huduma itokanayo na mifumo ya ekologia zinategemea hali halisi ambayo ni hali halisi ya matumizi ya ardhi kama kusingekuwa na program ya MKUHUMI+.

[37]Huduma itokanayo na mfumo ekologia' kwa mtizamo uu inamaanisha huduma ambazo sio za upunguzaji wa gesi joto

[38] Kwa kujumuisha bioanuwai na thamani za huduma zitokanazo na mfumo ekologia zimeainishwa kwenye mikakati ya taifa ya bioanuwai na mipango kazi (NBSAP), mchakato wa wazi unaosaidia shabaha za Mkataba wa Uwiano wa kibiologia 2010 au utekelezaji wa muongozo unaoendana na juhudi hizi kama Vidhibiti vya maendeleo vya benki (benki ya Dunia PO 4.04, vigezo vya utekelezaji vya IFC 6) maeneo muhimu ya bioanuwai, maeneo yenye thamani kubwa ya hifadhi za baioanuwai na mipangilio mingine ya uhifadhi.

[39] Kwa kujumuisha misitu ya asili na maeneo muhimu kwa ajili ya hifadhi ya bioanuwai na kipaumbele kwa ajili ya huduma zitokanazo na mfumo ekolojia na kusisitiza mipango yoyote itakayo panua misitu isiyo ya asili na atahri zake kwa bioanuwai na kipaumbele kwa huduma ya mfumo ekolojia.

MKUHUMI+ zinatunzwa na kuendelezwa	kipimo na kiwango ambacho kinakaribiana na kipengele/shughuli katika programu[40] 5.1.2 Malengo ya Programu ya MKUHUMI+ ni pamoja na kufanya mchango unaooneka katika kutunza na kuendeleza bioanuwai na huduma ya mfumo ekolojia. 5.1.3 Programu ya MKUHUMI+ ina ainisha na kutekeleza hatua zenye madhumuni ya kutunza na kuendeleza bioanuwai zilizoainishwa na huduma za mfumo ekolojia zilizopewa kipaumbele na zitakazothiriwa na programu ya MKUHUMI+ 5.1.4 Progamu ya MKUHUMI+ haipelekei kubadilishwa na misitu ya asili au maeneo mengine ambayo ni muhimu kwa kutunza na kuendeleza bioanuwai zilizoainishwa na huduma za mfumo ekolojia zilizopewa kipaumbele 5.1.5 Programu ya MKUHUMI+ inazalisha rasilimali[41] zaidi kwa ajili ya kutunza na kuendeleza bioanuwai na huduma za mifumo ekolojia.
5.2 Athari chanya na hasi za kimazingira za programu ya MKUHUMI+ zenye kipaumbele kwenye bioanuwai na huduma za mifumo ekolojia na athari nyingine zimetathminiwa pamoja na athari zilizotabiriwa na zile zilizohalisi.	5.2.1 Mpango wa ufuatiliaji na viashiria vimeanishwa kwa ajili ya upimaji wa bioanuwai na huduma za mfumo ekolojia iliyoainishwa na kupewa kipaumbele kuathirika na programu ya MKUHUMI+kwa kuzingatia elimu asilia na utafiti wa kisayansi kama itavyopaswa. 5.2.2 Kuna tathmini ya athari za kimazingira zilizotabiriwa na zilizohalisi za programu ya MKUHUMI+[42] na kuzinazohusisha watu wa jamii asilia, na jamii pamoja na wadau wengine kama inavyofaa.
5.3 Programu ya MKUHUMI+ imepokelewa kulingana na tabiri na tathmini zinazoendelea kupunguza athari hasi na kuendeleza athari chanya za kimazingira	5.3.1 Hatua za kuainisha na kukabiliana na athari za kimazingira zenye uhasi zimeingizwa katika kuunda kwa program ya MKUHUMI+ 5.3.2 Mrejesho kutokana na ufuatiliaji umetumika kuunda na kutekeleza hatua za kupunguza zaidi athari hasi za mazingira zilizo halisi wakati wa awamu ya utekelezaji wa program ya MKUHUMI+

[40] Kwa kujumuisha lakini sio tu katika maeneo muhimu ambayo yako hatarini au aina ya mimea/wanyama wasiopatikana mahali popote, kwa mlundikano muhimu au vyanzo vya idadi ya aina ya mimea/wanyama, kwa mifumo ekolojia na kwa huduma inayotokana na mifumo ekolojia kiuchumi, kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, umuhimu wa utamaduni au dini kwa wadau hususan jamii ya watu asilia na jamii iliyopo kisheria.

[41] Kuwa makini kwa mipango yoyote ya kupanua misitu ambayo sio ya asili na madhara yake kwa bioanuwai na thamani ya huduma ya mfumo ekologia.

[42] Kwa mfaano kupitia kwenye Mkakati wa tathmini ya mazingira au Tathmini ya athari za kimazingira

	5.3.3 Mrejesho unaotokana na ufuatiliaji unapelekea hatua za kuendeleza athari za kimazingira.

Kanuni 6: Wenye haki husika wote[43] na wadau wanashiriki kikamilifu na kwa ufanisi[44]katika programu ya MKUHUMI+	
Vigezo	**Muongozo wa viashiria**
6.1 Programu ya MKUHUMI+ ina ainisha na kuelezea haki na maslahi ya wenye haki wote na makundi ya wadau[45]na umuhimu wao katika programu ya MKUHUMI+.	6.1.1 Wenye haki na makundi ya wadau wameaninishwa wakiwemo watu wa jamii asilia, jamii iliyoko pale kisheria, kwa kuangalia kwa umakini mahitaji ya makundi maalumu yalio pembezoni na hatarini. 6.1.2 Haki na maslahi ya kila mwenye haki na kila kundi la wadau kuhusiana na programu ya MKUHUMI+ vimeanishwa na pamoja na vikwazo vilivyopo kwenye ushiriki wao, na umuhimu wao kwenye programu ya MKUHUMI+ umeanishwa. 6.1.3 Kuna utaratibu wa kuwezesha utakaotumika kwa kila atakayependa kutumia ili awe mwenye haki au mdau kulingana na haki na maslahi yao kuhusiana na programu ya MKUHUMI+
6.2 Wenye haki na makundi ya wadau wanaotaka kuhusishwa katika kuunda[46]utekelezaji[47] na kutathmini programu ya MKUHUMI+ wanahusishwa na kushirikishwa kikamilifu.	6.2.1 Mchakato na muundo wa kitaasisi umeanzishwa na unafanya kazi ili kuwezesha wenye haki wote na makundi ya wadau kushiriki kikamilifu katika kuunda, kutekeleza na kutathmini programu. 6.2.2 Kuna uwakilishi thabiti na wenye usawa wa makundi yaliyoko pembezoni na /au makundi yaliyoko hatarini katika hatua za mchakato wa ushirikishwaji wa wenye haki na wadau wakiwemo wanawake.. 6.2.3 Majadiliano juu ya programu ya MKUHUMI+ yanafuata hali halisi ya kijamii na kiutamaduni kwa njia zinazofaa na kufanyika katika maeneo yanayokubalika na wote.

[43] 'Wenye haki na makundi ya wadau husika' wameainishwa na programu ya MKUHUMI+ kulingana na kigezo 6.1

[44] Ushirikishwaji thabiti' unamaanisha ushawishi wenye maana kwa wenye haki na wadau wote wanaotaka kuhusishwa kwahakikisha wanakuwa na taarifa za awali kwa wakti mwafaka.

[45]Makundi ya wenye haki au wadau walio na haki zinazofanana au maslahi kuhusiana na programu ya MKUHUMI+

[46]ikijumuisha na maendeleo ya matumizi ya ardhi na mipango ya usimamizi wa misitu katika programu ya MKUHUMI+.

[47] 'Utekelezaji' unaeleweka kujumuisha mipango/ufanyaji wa maamuzi unaoendelea pamoja na utekelezaji wa shughuli.

	6.2.4 Serikali za mitaa zimehusika katika programu ya MKUHUMI+ pamoja na serikali kuu katika ngazi ya taifa na katika ngazi nyingine husika na wajibu na majukumu yao yameainishwa bayana. 6.2.5 Muundo na utekelezaji wa Programu ya MKUHUMI+ umefanyika kwa kuzingatia majadiliano yanayoendelea ya wenye haki na wadau kwa kuwashirikisha kwenye kuunda, kutekeleza na kutathmini programu. 6.2.6Wenye haki na makundi ya wadau husika wanapatarasilimali za kutosha kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika kuunda, kutekeleza na kutathmini programu ya MKUHUMI+
6.3 Wenye haki na makundi ya wadau husika wanaamua kwa namna inayothibitika, mchakato na njia watakayoshirikishwa na kuwakilishwa kuhusiana na programu ya MKUHUMI+ngatia taasisi za kisheria na za kimila.	6.3.1 Hatua za ushirikishwaji zitakazotumika na programu ya MKUHUMI+zimetayarishwa na kupitishwa na wenye haki na makundi ya wadau husika kwa kuzingatia ufanyaji kazi wa taasisi za kisheria na kimila. 6.3.2 Programu ya MKUHUMI+ inatambua na kuheshimu na haidharau mfumo wa ufanyaji maamuzi wa wenye haki na makundi ya wadau na taratibu hususan jamii ya watu asilia na jamii iliyopo kisheria. 6.3.3 Wenye haki na makundi ya wadau wanachagua wawakilishi wao watakao shiriki katika kufanya maamuzi juu ya programu ya MKUHUMI+. 6.3.4 Wawakilishi wa wenye haki na makundi ya wadau wanahakikisha kuwa wamehusishwa na wanawajibika kwa watu wanaowawakilisha, kuwataarifu juu ya jinsi gani programu ya MKUHUMI+ inavyoweza kuwaathiri na kuwezesha majadiliano na mrejesho.
6.4 Wenye haki na makundi ya wadau husika wana uelewa mzuri juu ya masuala muhimu kuhusiana na programu ya MKUHUMI+ na uwezo wa kushiriki kikamilifu	6.4.1 Usambazaji wa taarifa na shughuli nyingine za uhamasishaji zinahakikisha kuwa wenye haki na wadau husika wana uelewa mzuri juu ya programu ya MKUHUMI+ hususan jamii ya watu asilia na jamii iliyopo kisheria hasa walioko pembezoni na hatarini miongoni mwao. 6.4.2 Vikwazo vya kutoshiriki kikamilifu kwa wenye haki na makundi ya wadau husika katika kuunda, kutekeleza na kutathmini vimeainishwa na kushughulikiwa kwa njia ya kuwajengea uwezo unaofaa kulingana na mahitaji ya makundi yanayohusika.

6.5 Uundaji, utekelezaji na tathmini ya programu ya MKUHUMI+ inajengea kwenye, kuheshimu na kusaidia wenye haki na wadau utaalamu wa elimu asilia na mifumo ya usimamizi pamoja na ile ya jamii ya watu asilia na jamii iliyopo kisheria.	6.5.1 Utaratibu umeundwa ili kuainisha elimu asilia, ujuzi na mifumo ya usimamizi ya muhimu katika programu ya MKUHUMI+ 6.5.2 Programu ya MKUHUMI+ inajengea kwenye na kuheshimu kama inavyotakiwa elimu na ujuzi asilia pamoja na mfumo wa usimamizi uliyoainishwa na wenye haki na wadau husika katika kupanga, kutekeleza na kutathmini 6.5.3 Pale ambapo elimu asilia, ubunifu na ufanyaji kazi wa jamii ya watu asilia na jamii iliyopo kisheria inatumika, kurekodiwa au kumalizwa, hii ni katika hali ya kuwa huru, kuwa na taarifa mapema na kuridhia kulingana na viwango vya kimataifa[48]
6.6 Kuna mfumo wakupata na kushughulikia malalamiko na migogoro kikamilifu kuhusiana na muundo, utekelezaji na tathmini ya programu ya MKUHUMI+.	6.6.1 Kuna utaratibu uliowazi, usiopendelea na unaofikiwa na kila mtu umeundwa ili kushughulikia malalamiko na migogoro inayoibuka wakati wa uundaji, utekelezaji na tathmini ya programu ya MKUHUMI+ pamoja na taratibu za kusikiliza, kushughulikia na kutatua malalamiko ya wenye haki na wadau katika kipindi maalumu kilichokubalika. 6.6.2 Utaratibu wa utatuzi wa malalamiko na migogoro umetangazwa kwa wenye haki na wadau wote. 6.6.3 Wenye haki na wadau wote wana taarifa juu ya na wanaweza kufikia njia za kimataifa za kutatua malalamiko yanayohusiana na taratibu za utekelezaji wa taasisi za kimataifa na/au makubaliano ya kimataifa au taasisi nyingine,
6.7 Wenye haki na wadau wanapata ushauri wa kisheria na uelewa wa taratibu za kisheria zinazohusika pamoja na kuelewa matokeo ya kisheria na ya kifedha kuhusiana na programu ya MKUHUMI+	6.7.1 Huduma ya ushauri wa kisheria inapatikana kwa wenye haki na wadau ili kuwashauri juu ya taratibu za kisheria na matokeo kisheria na kifedha kuhusiana na programu ya MKUHUMI+

[48] Mfano Mkataba wa Uwiano wa Kibiolojia,

Kanuni 7: Wenye haki na wadau wote wanapata taarifa sahihi na kwa muda muafaka ili kuwawezesha kufanya maamuzi na utawala bora kwenye programu ya MKUHUMI+	
Vigezo	**Muongozo wa viashiria**
7.1 Taarifa za kutosha juu ya programu ya MKUHUMI+ zinapatikana kwa umma ili kuendeleza uhamasishaji na utawala bora kwa ujumla	7.1.1 Taarifa ya kutosha juu ya programu ya MKUHUMI+ inapatikana kwa umma na wenye nia ya kupata taarifa miongoni mwa umma pamoja na taarifa juu ya uundaji, utekelezaji, tathmini, pamoja na tathmnini za athari za kijamii na kimazingira, mgawanyo wa manufaa, bioanuwai na huduma za mifumo ekologia, na haki ya ardhi, mipaka na rasilimali 7.1.2 Sera za serikali zinasaidia wadau kupata taarifa kwa uhuru na kwa muda mwafaka juu ya programu ya MKUHUMI+ pamoja na taarifa ya haki ya ardhi, mipaka na rasilimali.
7.2 Wenye haki na wadau wana taarifa wanayoihitaji kuhusu programu ya MKUHUMI+ na inayotolewa kwa njia sahihi ya kiutamaduni na kwa muda unaofaa, ili washiriki kikamilifu katika uundaji, utekelezaji na tathmini, pamoja na taarifa muhimu kuhusu hatari na fursa zilizopo za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na hatari za kimazingira, maana ya matokeo ya kisheria, na mazingira ya kidunia na ya kitaifa.	7.2.1 Wenye haki na wadau wanajua ni taarifa gani inapatikana kuhusu programu ya MKUHUMI+ na namna ya kuipata. 7.2.2 Njia bora zaidi ya usambazaji wa taarifa juu ya programu ya MKUHUMI+ zimeainishwa na kutumika kwa kila mwenye haki na makundi ya wadau. 7.2.3 Wenye haki na wadau wanapata taarifa inayotakiwa juu ya programu ya MKUHUMI+ pamoja na matokeo ya ufuatiliaji na tathmini,hatari na fursa zilizopo za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kimazingira, maana ya matokeo ya kisheria , fursa za ushiriki katika taratibu ufanyaji wa maamuzi, njia za malalamiko na hali ya kidunia, kitaifa na ya ngazi ya chini 7.2.4 Jamii ya watu asilia na jamii nyingine inayoishi kisheria pamoja na makundi yaliyoko pembezoni na/au yaliyoko hatarini miongoni mwao, wanaweza kupata taarifa wanayohitaji juu ya programu ya MKUHUMI+ katika mfumo wanao elewa.
7.3 Wawakilishi wa wenye haki na makundi ya wadau wanakusanya na kusambaza taarifa juu ya programu ya MKUHUMI+ kutoka na kuwapelekea watu wanaowawakilisha kwa njia sahihi na kwa wakati muafaka.	7.3.1 Wawakilishi wa wenye haki na makundi ya wadau wanakusanya na kusambaza taarifa zote muhimu zinazohusiana na programu ya MKUHUMI+ na kuwapelekea watu wanaowakilisha. 7.3.2 Taratibu zimewekwa ili kuhakikisha kwamba wenye haki na wadau wanapata na kutoa taarifa zote muhimu kuhusiana na programu ya MKUHUMI+ kupitia kwa wawakilishi wao.

7.4 Taarifa zipo na zinasambazwa kuhusiana na programu ya MKUHUMI+ kwa muda muafaka ili kuwezesha wenye haki na wadau kutoa mrejesho kwa wawakilishi wao na kuheshimu muda uliopangwa ili kushiriki kwenye kufanya maamuzi.	7.4.1 Taarifa ipo na inasambazwa juu ya programu ya MKUHUMI+ nakuruhusu muda wa kutosha kati ya usambazaji wa taarifa na ufanyaji wa maamuzi ili kuwezesha wenye haki na wadau kuratibu maamuzi yao.
7.5 Programu ya MKUHUMI+ inatoa rasilimali za kutosha ili kuweza kutoa na kukusanya taarifa kwa muda muafaka na kwa njia sahihi.	7.5.1 Kuna rasilimali za kutosha ili kuhakikisha kwamba taarifa muhimu juu ya programu ya MKUHUMI+ zinasambazwa kwa na kukusanywa kutoka kwa wenye haki na wadau wote ili kuratibu majibu yao.

Kanuni 8: Programu ya MKUHUMI+ inakubaliana na sheria za kitaifa zinatotumika[49] na za ngazi ya chini mikataba, kanuni na makubaliano ya kimataifa[50]	
Vigezo	**Muongozo wa viashiria**
8.1 Programu ya MKUHUMI+inakubaliana na sheria ya ngazi yachini, sheria ya kitaifa na sheria, kanuni na makubaliano ya kimataifa yaliyoridhiwa na kutumika na nchi.	8.1.1 Makubaliano ya kimataifa, mikataba na vyombo vinginevilivyoridhiwa na kutumika na nchi vinavyoendana na programu ya MKUHUMI+ zimeainishwa. 8.1.2 Sheria za kitaifa na zingine za nchi muhimu kwa programu ya MKUHUMI+ zimeainishwa 8.1.3 Programu ya MKUHUMI+ inatambua na kuheshimu haki za binadamu[51] za jamii ya watu asilia, jamii nyingine kisheria pamoja na wanawake na makundi yaliyo pembezoni kama yalivyoainishwa na sheria ya kitaifa na kimataifa. 8.1.4 Eneo lolote ambalo muundo na/utekelezaji wa programu ya MKUHUMI+ hauendani au hautoendana na sheria za kitaifa au za ngazi ya chini na mikataba, kanuni na makubaliano[52] ya kimataifa litaainishwa na [53] na

[49] Sheria za nchi zinajumuisha kanuni zote za kisheria zinazotolewa na vyombo vya serikali vyenye mamlaka isiyozidi ya kitaifa kama idara, manispaa na za kimila.

[50] Ikijumuisha lakini sio tu Azimio la kimataifa kuhusu haki za binadamu, Muongozo na makubaliano ya Umoja wa Mataifa juu ya Mabadiliko ya Tabia nchi, makubaliano ya uwiano wa kibiolojia, Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya haki za jamii ya watu asilia, Makubaliano juu ya uondolewaji wa ubaguzi wa kila aina dhidi ya wanawake, makubaliano ya kimataifa juu ya mashirika ya wafanya kazi 169

[51] Ikijumuisha haki ya kujipangia kwa jamii ya watu asilia, na mahitaji ya hali ya kuwa huru na kupata taarifa kamili kabla ya kuridhia kuhusiana na kuanza kutumia kwa sheria au hatua za utawala pamoja na taratibu nyingine muhimu ambazo zitaathiri haki.

[52] Ikijumuisha kuheshimu haki ambazo zimeelezewa kwenye mikataba, makubaliano na vyombo vingine.

	kufuatiliwa na hatua zinazofaa zimechukuliwa kujihakikishia utekelezaji.
8.2 Pale ambapo sheria za ngazi ya chini au za kitaifa haziendani na viwango vilivyowekwa, taratibu za kupitia zifanyike ambazo zinapelekea mpango wa kupata ufumbuzi wa maeneo ambayo yanatofautiana.	8.2.1 Taratibu za kupitia zimeanzishwa kushughulikia maeneo yanayotofautiana kati ya viwango na sheria za nchi au za kitaifa pamoj na sheria zilizotangulia na marekebisho ya muongozo wa sheria ambayo yanaweza kutokea wakati wa utekelezaji wa programu ya MKUHUMI+.
8.3 Wenye haki[54] na wadau husika wana uwezo wa kuelewa, kutekeleza na kufuatilia mahitaji ya kisheria kuhusiana na programu ya MKUHUMI+	8.3.1 Wenye haki husika na wadau wana uwezo wa kuelewa, kutekeleza na kufuatilia mahitaji ya kisheria kuhuisiana na programu ya MKUHUMI+

[53] Kutumia njia zinazofaa kufanya tathmini ikiwemo tathmini ya athari kwa haki za binadamu

[54] Haki za wadau husika katika vigezo hizi inamaanisha wale wenye majukumu ya kutekeleza na kufuatilia vyombo vya kisheria.

Maana ya maneno

Haki ya hewa ukaa inamaanisha haki ya kuingia mkataba na vipengele vya kuuza na kununua kwa ajili ya kuhamisha miliki ya uzalishaji na upunguzaji wa gesi joto au kuondoa na kuendeleza kiasi na kiwango cha hewa ukaa.

Gharama, manufaa na hatari za programu ya MKUHUMI+ zinajumuisha zile ambazo ni za moja kwa moja na zile zisizo za moja kwa moja na zina vipengele vya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi. Gharama zinajumuisha zile ambazo zinapatikana kwa kupoteza fursa. Gharama, manufaa na hatari zote zinaringanishwa na hali halisi iliyopo ambayo ni matumizi ya ardhi yanayoonekana kama hakuna programu ya MKUHUMI+.

Tafsiri kwa nchi maalumu inamaanisha tafsiri katika ngazi ya utawala unaoongoza programu ya MKUHUMI+

Vigezo ni mambo 'yaliyomo' katika kiwango ambacho kimepangwa na kinahitaji kufikiwa ili kuweza kufikia kanuni. Inawezekana kuthibitisha vigezo moja kwa moja lakini mara nyingi vinaelezwa zaidi na viashiria.

Haki za kimila kwa ardhi na rasilimali inamaanisha mifumo ya matumizi ya ardhi na rasilimali ya jamii kwa muda mrefu na kuwa na sheria za kimila, kanuni, miiko na mambo ya asili kwa jamii ya watu asilia na jamii nyingine ikiwemo matumizi ya msimu au ya kurudiwa kuliko kuwa na haki miliki ya ardhi na rasilimali kisheria inayotolewa na serikali

Huduma za mifumo ekologia kwa mtizamo huu zinamaanisha huduma nyingine mbali na za upunguzaji au kuondoa gesi joto

Uthabiti wa programu ya MKUHUMI+ unamaanisha kwa kiwango gani uzalishaji wa hewa ukaa umepunguwa na malengo mengine ya programu yalivyofanikiwa.

Ufanisi unamaanisha kufikia shabaha iliyowekwa kwa gharama nafuu, kwa juhudi ndogo na kwa muda mfupi.

Usawa na **usawa usio na upendeleo** vinamaanisha ile tu kutofungamana na upande wowote kwa wahusika wote

Muongozo wa viashiria unamaanisha vipengele maalumu kwa kila kigezo. Kutakuwa na utaratibu wa tafsiri maalumu kwa kila nchi ili kuanzisha viashiria vitakavyo endana na mfumo wa nchi husika.

Kukamilika na **ukamilifu** kama ambavyo imetumika katika ushirikishwaji kikamilifu inamaanisha katika hatua zote.

Ushirikishwaji thabiti unamaanisha ushawishi ulio na maana kw wenye haki na makundi ya wadau husika wanaotaka kuhusishwa kwenye mchakato, na kujumuisha majadiliano na hali ya kuwa na taarifa na kuridhia.

Utawala bora unajumuisha upatikanaji, ushiriki wa watu, uwazi, uwajibikaji, utawala wa sheria, utabirikaji, haki ya sheria na uendelevu.

Utekelezaji unajumuisha mipango inayoendelea/ufanyaji wa maamuzi pamoja na utekelezaji wa shughuli

Viashiria ni vipengele vinavyohesabika na visivyohesabika vinavyoweza kufanikishwa na kuthibitiwa kuhusiana na vigezo

Shughuli za kimaisha zinatokana na uwezo na rasilimali jamii, kiutamaduni, watu, kifedha, maliasili, rasilimali za miundombinu na uwezo wa kisiasa.

Sheria za ndani nchi inajumuisha kanuni zote zinazotolewa na vyombo vya serikali ambazo utawala wake wa utekelezaji haufiki katika ngazi ya taifa kama vile kanuni za idara, manispaa, na za kimila.

Makundi ya watu walioko pembezoni ni wale ambao mara nyingi wana nafasi ndogo ya kushawishi juu ya hatua za ufanyaji wa maamuzi. Kuwa pembezoni kunahusishwa na jinsia, ukabila, hali ya kiuchumi kwa jamii na/au dini. Viwango vya MKUHUMI+ vya kijamii na kimazingira kwa kipekee zimeitatumia njia ya kutofautisha ambayo inalenga kuainisha, na inapobidi, kupambana na upembezoni kwa kila namna.

Kanuni ni mpango katika ngazi ya kiwango unaoelezea juu ya malengo ya kiwango na kuwekea mipaka. Ni maneno ya msingi juu ya matokeo tarajiwa na hayategenezwi kwa ajili ya kuthibitishwa.

Programu ya MKUHUMI+ inajumuisha malengo, sera na hatua zilizotayarishwa kwa ajili ya programu na sera nyingine zinazosaidiana.

Rasilimali zinaeleweka kujumuisha huduma za mifumo ekologia zinazotokana na rasilimali hizi.

Wenye Haki na wale ambao haki zao zinaathiriwa na programu ya MKUHUMI+ na ‘wadau’ ni wale ambaomaslahi yao yanaweza kuathiriwa na programu.

Viwango vinajumuisha kanuni,, vigezo na viashiria vinavyoelezea masuala ya muhimu kwa ajili ya mahitaji ya kiutendaji ya kijamii na kimazingira

Makundi ya watu walioko hatarini ni wale ambao hawawezi kupata kwa urahisi mali ambapo uhakika wa maisha unajengwa. (kijamii, kiutamaduni, kifedha, kiasili, mali zinazo/zisizoweza kuhamishika na kisiasa) na /au kuwa katika hatari ya juu ya kupata mishtuko kama mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaweza kuathiri mali hizi na uwezo wa jamii kutumia mali hizo. Utegemezi wa misitu ni moja ya sababu muhimu inayoathiri watu walioko hatarini hususan pale ambapo programu ya MKUHUMI+ itakapobadilisha upatikanaji wa rasilimali. Wakati mwingine watu waliopembezoni wanakuwa hatarini zaidi, mfano waliopembezoni kutokana na masuala ya kijinsia hali nyingi upembezoni unazidiwa na hali ya uhatari mf jinsia